

Mamlaka ya kila kanisa la mahali Fulani

Mamlaka ya juu sana katika kanisa ni mzee, sio askofu, siyo mkuu fulani au chochote. Mungu anashughulika na huyo mzee na hilo kanisa. sasa, analipa kanisa lake ujumbe wake, na kile anacho kihitaji [1]

Fundisho la wanikolai

Ufunuo 2:15, “vivyo hivyo wewe nawe unao watu wayashikao mafundisho ya wanikolai, ambayo ninayachukia vilevile.

”Utakumbuka ya kwamba nilielezea katika wakati wa Efeso kuwa lile neno, Nikolai, linatokana na maneno mawili ya kiyunani: Nikao ambalo linamaanisha kutiisha, na lao ambali linamaanisha washirika. Nikolai maana yake ni “kuwatiisha washiriki.” Sasa kwa nini hili ni jambo baya sana? Ni baya kwa sababu Mungu hajaliweka kamwe kanisa lake mikononi mwa viongozi walio pigiwa kura wanaoongozwa na mawazo ya kisiasa. Ameliweka Kanisa lake katika ulinzi wa watu walio chaguliwa na Mungu, waliojazwa Roho, watu wanaoliishi Neno na kuwaongoza watu kwa kuwalisha Neno. Yeye hajawatenganisha watu katika madaraja hivi kwamba umati uongozwe na ukasisi mtakatifu. Ni kweli ya kwamba uongozi lazima uwe mtakatifu, lakini pamoja na hayo kusanyiko lote liwe takatifu. Isitoshe, hakuna mahali katika Neno ambapo makasisi ama wahudumu ama watu wa namna hiyo hupatanisha kati ya Mungu na watu, wala hakuna mahali ambapo wanatenganishwa katika kumwabudu kwao Bwana. Mungu anataka wote wampende na kumtumikia pamoja. Unikolai huharibu amri hizo na badala yake huwatenganisha wahudumu na watu na kuwafanya viongozi wawe mabwana-watawala badala ya kuwa watumishi. sasa. Fundisho hili lilianza kama tendo katika wakati wa kwanza. yaonekana kwamba shida ilianza katika maneno mawili; “wazee wa kanisa” (makasisi) na “wachungaji” (maaskofu). Ingawa maandiko yanaonyesha kwamba kuna wazee kadha wa kadha katika kila kanisa, baadhi ya watu walianza (miongoni mwao akiwemo Ignatio) kufundisha kuwa wazo la askofu lilikuwa kwamba yeye ni mtu mwenye cheo kikubwa ama mwenye mamlaka na amri juu ya wazee. Sasa ukweli wa mambo ni

kwamba neno “Mzee” linaonyesha mtu huyo ni nani, ambapo neno “Askofu” linaonyesha huduma ya mtu yuyo huyo. mzee ni mtu mwenyewe. askofu ni huduma ya huyo mtu. “mzee” siku zote limekuwa na kila mara litakuwa tu likimaanisha umri wa mtu katika Bwana. Yeye ni mzee, si kwasababu amechaguliwa kwa kura ama amewekewa mikono, n.k., bali ni kwasababu ana umri mkuu ZAIDI. Yeye amekolea zaidi, amefundishwa, si mwanafunzi, ni mtu anaye tumainiwa kwa sababu ya ujuzi na uthabiti wa ujuzi wake wa Kikristo wa siku nyingi. bali sivyo, maaskofu hawakushikilia nyaraka za Paulo, bali walipendelea kwenda kwenye taarifa ya Paulo ya wakati alipowaita wazee kutoka Efeso kwenda Mileto katika Matendo 20. katika kifungu cha 17 taarifa hiyo inasema, “wazee” waliitwa na baadaye katika kifungu cha 28 wanaitwa waangalizi (maaskofu.) nao hawa maaskofu, (bila shaka wakiwa na mawazo ya kisiasa na wenye shauku ya kutaka madaraka) walisisitiza ya kwamba Paulo alikuwa akimaanisha kuwa “waangalizi” walikuwa ni zaidi ya wazee wa mtaa ambaye ana mamlaka rasmi katika kanisa lake mwenyewe tuu. Kwao askofu alikuwa sasa mtu mwenye mamlaka juu ya viongozi wengi wa mitaa. Wazo kama hilo halikuwa la kimaandiko wala la kihistoria, hata hivyo hata mtu wa hadhi kama Polikapu aliegemea kwenye mwongozo kama huo. Kwa hiyo, lile lililoanza kama tendo katika wakati wa kwanza lilifanywa fundisho la kweli na ndivyo ilivyo sasa. maaskofu wangali wanadai mamlaka ya kuwaongoza watu na kuwatendea vile wapendavyo, wakiwaweka mahali wao wapendapo katika huduma. Jambo hili linakaidi uongozi wa Roho Mtakatifu aliyesema, “nitengeeni Paulo na Barnaba kwa kazi ile niliyowaitia.” Hili ni pinga-Neno na ni pinga-Kristo. Mathayo 20:25-28, [2]

Sasa, kumbuka sababu iliyoacha nikashikana na kanisa la baptisti ilikuwa ni uhuru wa kimaamuzi wa kila kanisa la mahali fulani nayo niliwaza ni utaratibu wa kimitume, unaona? Siyo kama wabaptisti tulio nao pale.....hata sihudhuri kwenye ibada zao, lakini kanisa la kibaptisti siyo dhehebu, halipaswi kuwa. lakini sasa ni dhehebu, lakini halikupaswa kuwa dhehebu. Ni ushirika wa kindugu, na kila kanisa mahali fulani lina maamuzi yake. na kama Mungu ataenda kutoa ujumbe kwa mtu wake, Mzee wake, ambayo ni ---kutokana na Biblia, mamlaka ya juu sana ya ofisi katika kanisa la mahali fulani ni mzee. Na sasa, kupitia kwa huyu mzee inakuja kwa mkuu wa mkoa, na kadhalika na kuja kwa askofu, na imeandikwa “Tunaamini kipindi hiki. Hivyo sasa” [3]

Usiweke askofu juu ya hilo.mwachie Roho mtakatifu asimamie hilo unaona? Roho Mtakatifu ametumwa kuondoa magugu na vinginevyo nje; siyo vile askofu anavyofikiri, au mzee mkuu au na kadhalika.

Inamchukuwa Roho Mtakatifu kuliweka kanisa katika hali yake. Yeye alikuwa ni lile Neno kamilifu kama tutakavyoona.

Adamu alikuwa na chaguo lake; lile Neno na aishi, au asiliamini Neno moja na afe. Tunao uchaguzi sawa na yeye, kwa sababu ni lazima iwe kama Mungu alimuweka Adamu kwenye Neno, na Neno pekee, Halafu atuweke sisi kwenye kanuni au kitu cha aina yoyote ya kanuni, hapo Mungu atakuwa siyo mwenye haki katika hukumu zake; hiyo haipasi katika Utakatifu wake wala katika mamlaka yake ya maamuzi .Lakini inapasa katika mamlaka yake ya maamuzi kuona kuwa anamuweka kila mtu katika msingi ule ule. Na Yeye ni Mungu na habadiliki. Mungu alichofanya kwanza, ataendelea kikifanya hicho hicho. kamwe habadilishi utaratibu wake. Jambo pekee, Yeye hulikuza hilo,lakini kamwe halibadilishi hilo. Jambo hilo hilo linaendelea [4]

Ni jambo rasmi kulingana na kanisa. Katika kanisa letu, kanisa ndilo lenye mamlaka.kanisa huondoa ama huingiza wadhamini, kanisa humwondoa mchungaji, ama linamweka mchungaji, chochote kile, ni kanisa katika kila jambo. Huko ni kuenenda kimitume. Hivyo ndivyo ilivyo fanyika katika wakati wa Biblia. Kwa hiyo, tunajisikia ya kwamba hakuna mtu mmoja peke yake, basi, ni kiongozi wa mabavu ama chochote kile kanisani. hatutaki jambo hilo. kila mwanamume, kila mtu, mimi mwenyewe, katika kumchagua mtu yeyote, ama kura moja tu, si kile ninachosema; ni vile kanisa linavyosema, unaona, vile kanisa linavyosema katika ule mwili. Mnapenda jambo hilo? [kusanyiko linasema , “Amina.”-Mh.] Loo, nafikiri hilo ni la kimaandiko kabisa. hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. [5]

Ninyi wote mmelipigia kura kwa asilimia mia moja kwa hiyo tumeshikilia sawa hilo unaona?

Kanisa lina uhuru wa kufanya maamuzi yake. Kile kanisa linachosema ndio ambacho Wadhamini au mwingine yeyote Yule wadhamini tu, kila mmoja anayo kura moja. Mchungaji ana kura moja tu. Ni kanisa kwa ujumla wake linanena. Hivyo ndivyo tu. Natunapenda hilo, kwa sababu hatuna askofu wakuwatawala au mtu mkuu fulani wa

kutuambia hili au lile au linguine. Ni Roho Mtakatifu ndani ya kanisa ambaye ananena. Mimi nalipenda hilo, na hilo ni zuri sana. [6]

Na hata hivyo, wakati ninamzungumzia mtu fulani hapa kuzunguka nchi hii mahali fulani ana hatia hapa mimbarani. Unapaswa kuliweka vizuri hilo pamoja na mimi -----, hivyo ni sawa ----- ndivyo hakika. Sasa nawataka ninyi..... imesema kitu fulani juu ya baraza la mashemasi. Baraza la mashemasi halina hata kitu kimja kuhusu utendaji wa huyu mchungaji. Hapana Bwana, kusanyio kwa ujumla wake ndio lenye mamlaka yote. Siyo Baraza la mashemasi ni polisi tu, hapa kanisani, kule kuweka utaratibu/utulivu na kadhalika. Lakini inapokuja katika kanuni, kanisa lote inabidi liseme hivyo. Hili kanisa limejengwa katika msingi wa uhuru wa maamuzi wa kanisa la mahai fulani kwa hiyo sina cha kusema katika kumuondoa huyu mchungaji au kumuweka mwingine hapa. Mimi ninamiliki hili eneo. Nimelitoa kwa kanisa. Ninyi wote hapa ndio kanisa. Ninyi ndio mnayo mamlaka, ninyi ndiyo wenye uhuru wa maamuzi, Mtakavyo, ni Roho Mtakatifu katika hilo kanisa, na jambo moja lipo ninalomiliki hilo eneo. Nimelitoa kwa kanisa kama Linachagua mchungaji wao wenyewe sina chochote cha kufanya na hilo. Njia pekee huyu mchungaji anavyoweza kuondoka, ni mchungaji aamua mwenyewe kuondoka au kura za watu wengi ziseme” tumbadilishe mchungaji na hiyo ndiyo njia pekee hakuna Baraza la mashemasi liwezalo kufanya hivyo. Baraza la mashemasi linaweka utaratibu tuu katika kanisa na mambo mengineyo.

Wale wadhamini hawana chochote cha kufanya na hilo. Wanahusika tu na ukarabati wa majengo ya kanisa na hawafanyi hilo, mpaka baraza lote la mshemasi likutane na liseme, “ Tuta jenga hili au tutafanya hivi”. Hapo sasa wanamuuliza mtunza hazina kama wanazo pesa za kufanya hivyo. Ndiyo bwana [7]

Lakini ninaamini juu ya mamlaka kuu ya kusanyiko la mahali fulani, ndio liache kila kanisa lijitegemee lenyewe, lichague wachungaji wake, lichague mashemasi wake na wowote wale wao. Na hapo askofu juu yake kama Roho Mtakatifu anataka kuzungumza chochote na hilo kanisa, hawana haja ya kumuuliza mtu fulani kama wafanye hili au lile ni juu ya huyu mtu binafsi ambaye anaguswa na Roho Mtakatifu. Nionyeshe mimi kwa Biblia,

kipi kikubwa katika Biblia zaidi ya mzee wa mahali fulani katika kanisa la mahali pale? Hivyo kweli ndiyo Bwana, ule uhuru wa kufanya maamuzi wa kanisa la mahali fulani kila kanisa likijitegemea lenyewe..... Sasa ushirika wa ndugu, hilo ni la ajabu. Makanisa yote yanapewa kuwa katika ushirika wa ndugu kama hivyo pamoja, lakini uhuru wa maamuzi wa kanisa la mahali fulani. [8]

Sasa, kama kuna kitu unachojua ambacho siyo sahihi mtu fulani/binafsi au mtu au chochote, unawajibika na utajibu mbele za Mungu kama husahihishi hicho kitu, Ninyi kanisa sasa kumbukeni hilo haliko mabegani mwangu tena hiko kwenu. Na kitu chochote ambacho siyo sahihi ndani ya kanisa, Mungu atakufanya wewe ujibu kwa ajili yake hivyo ni sawa. Hivyo ndivyo anavyoendesha kanisa lake. Hivyo ndivyo ilivyo katika Biblia. Huo ndio utaratibu katika Biblia, huo ni uhuru wa maamuzi wa kanisa la mahali fulani mchungaji ndiye mkuu/kichwa. Hivyo ni sawa Amina!

Kwa hivyo, hakuna mtu mmoja pekee aliye na chochote cha kufanya katika hili. Ni lile kusanyiko lote la watu wote ndiyo Bwana. Kama ishirini wanamkubali na ishirini na moja hawamkubali inabidi aondoke na hivyo hivyo kinyume chake, unaona? Hivyo ndivyo, ni ile mamlaka ya kanisa la mahali fulani na sasa kila mmoja wa washirika anayo haki ya kutoa mawazo katika kanisa, kitu chochote kikienda siyo sahihi, hapo sasa wanaweza wakaja pamoja na jambo pekee wawezalo kuhakikisha kuwa hakuna kitu chochote kinachozuia kuendelea kwa kanisa.

Lakini ukamilifu na mamlaka yote ya kanisa ni mchungaji. Soma hilo katika Biblia angalia hilo kama siyo utaratibu wa Biblia. Hivyo ni sahihi kabisa. Hakuna mtu ambaye yuko juu ya mchungaji si sihusiki na chochote ndugu Neville anachotaka kufanya hapa. Hiyo ni juu yenu na ndugu Neville. [9]

Na sasa kanisa la Mungu ndiyo mahali pa juu sana pa hukumu. Mchungaji ndiye mwenye mamlaka ya juu katika kanisa. Mzee ndiye mkuu katika kanisa la kimitume, nje ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu analeta ujumbe wake moja kwa moja kwa mzee na mzee anatoa kwa watu.

Nukuu za kiingereza

- [1] Mara moja tena Bwana (63 -0120E), Para 75
- [2] Wakati wa kanisa wa pergamo, Kitabu cha nyakati 7 uk 197
- [3] Ripoti ya safari ya India (57-0126B), Aya E-15
- [4] Wakati wa mavuno (64 - 1212) 115-117
- [5] Hisia kuu (59 – 1227E), Aya 16
- [6] Ufunguo wa mlango (62 - 10071), Aya 8
- [7] Waebrania 7 sehemu ya 2 na utaratibu wa kanisa (57-0922), Aya 276 – 282,292
- [8] Waebrania 5 na 6 (57-0908M), Aya 26
- [9] Utaratibu wa kanisa (58 -1007) utaratibu wa kanisa mfundisho – uk 1199

Jiwe la kujengea la kiroho nambari 182 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendstr. 69.D-75328 Schomberge Germany Simu (+49) 2357613 Fax 72353306.

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk.) Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: Chaelika@livel.com
Cellphone: 0784 704299/ 0713230098